Tangazo hili limeidhinishwa na Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA)

**TANGA CEMENT PLC**

(Imesajiliwa chini ya Sheria ya Kampuni ya Tanzania namba 212 ya mwaka 2002 kama kampuni yenye dhima ya ukomo, cheti cha usajili namba 5068 na kuorodheshwa katika Soko la Hisa la Dar es Salaam)

---

**TAARIFA KWA UMMA**

**MATOKEO YA MAUZO YA HISA STAHIKI ZA TANGA CEMENT PLC**

---

Tanga Cement PLC inatoa taarifa kwa umma kuwa mnamo tarehe 11 Septemba 2025, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) katika kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana, Sura ya 79 ya Sheria za Tanzania, iliidhinisha Waraka wa Matarajio wa kampuni ya Tanga Cement kuuza Hisa Stahiki 127,342,090 kwa wanahisa wake kwa bei ya Shilingi 1600 kwa kila hisa, katika uwiano wa hisa mbili (2) mpya kwa kila hisa moja (1) aliyonayo mwanahisa.

## MATOKEO YA MAUZO YA HISA STAHIKI

Mauzo ya Hisa Stahiki yalifunguliwa Jumatatu tarehe 29 Septemba 2025 na kufungwa Ijumaa tarehe 24 Oktoba 2025, ambapo maombi yenye thamani ya shilingi bilioni 203.74 yamepokelewa kama ilivyotarajiwa, sawa na mafanikio ya asilimia 100.

## MUHTASARI WA MAUZO

Muhtasari wa takwimu muhimu za mauzo ni kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| Mtoaji | Tanga Cement PLC |
| Maelezo | Hisa Stahiki |
| Idadi ya Hisa Stahiki zilizotolewa | 127,342,090 |
| Thamani ya Maombi yaliyopokelewa | Shilingi 203,747,344,000 |
| Kiwango cha matokeo | 100% |
| Bei ya hisa | Shilingi 1600 kwa hisa |
| Uwiano | Hisa mbili (2) mpya kwa kila hisa moja (1) aliyonayo mwanahisa |

## MAELEZO YA ZIADA

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Tanga Cement PLC au Mshauri Kiongozi (iTrust Finance Limited) kupitia barua pepe: tangarightsissue@itrust.co.tz au +255 659 071 777

## TAREHE ZA MATUKIO MUHIMU

Tafadhali zingatia tarehe zilizopendekezwa kufuatia ufungaji wa ofa:

| **Maelezo** | **Tarehe** |
|---|---|
| Tarehe ya kutaarifiwa Wawekezaji (kupitia baruapepe/simu) | Alhamisi, Novemba 20, 2025 |
| Tarehe ya kuorodhesha hisa stahiki kwenye soko la hisa la Dar es Salaam (DSE) | Alhamisi, Novemba 27, 2025 |

**SHUKRANI**

Menejimenti ya Tanga Cement PLC inatoa shukrani za dhati kwa taasisi zote zilizofanikisha uuzwaji wa Hisa Stahiki. Taasisi hizi ni pamoja na Bodi na Uongozi wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA); Bodi na Uongozi wa Soko la Hisa la Dar Es Salaam (DSE); ); Mshauri Kiongozi, iTrust Finance Limited; Mshauri wa Masuala ya Kisheria, Joachim & Jacobs Attorneys; pamoja na Mhasibu, Deloitte & Touche. Aidha, Bodi ya Wakurugenzi ya Tanga Cement PLC inatoa shukrani kwa wanahisa wote kwa imani waliyonayo kwa kampuni hii na ushirikiano wao mkubwa katika zoezi hili hadi kufanikiwa kwa kiasi kikubwa.

**Imetolewa na:**
**Mkurugenzi Mtendaji,**
**Tanga Cement PLC,**
**Pongwe , Barabara ya Tanga – Korogwe,**
**S.L.P 5053,**
**Tanga, Tanzania**

**Tarehe: 20 Novemba 2025**

Tangazo hili limetolewa kwa idhini ya Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa mujibu wa kanuni za Masoko ya Mitaji za Matangazo, G.N. Namba. 15 ya mwaka 1997.